**Kila mtu ana malaika (06) - Ushauri nasaha kuhusu ukimwi**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

## Wahusika

Jet
Annie
Angela
Djamila
Mganga wa kienyeji - mwanamme mwenye umri wa miaka 50

## Utangulizi

Karibu katika kipindi kingine cha sikiliza ujifunze kwenye sehemu nyingine ya mchezo wa kuigiza Malaika wa kila mtu.

Msichana Angela anakabiliwa na mikasa ya kupata mimba isiyo ya kutarajia lakini anayaweka siri matokeo yake juu ya uchunguzi wa virusi vya HIV, hajamwambia hata mamake ambaye ana hasira juu ya ujauzito wa mwanawe na aibu alomtia. Djamila nae anajaribu kuidadisi familia yake juu ya upimaji virusi vya HIV lakini hakuna aliye tayari kumjibu, ila mjomba wake anampa ushauri dhidi ya kujihusisha katika kufanya mapenzi.

Katika kisa cha leo msikilizaji, Angela anachukua hatua ya kijasiri ya kubadili maisha yake, wakati rafiki yake Annie na mpenzi wake wa zamani wakikabiliwa na tatizo jingine.

Je nini kitatokea, ungana nasi katika mchezo Malaika wa kila mtu.

## SURA YA KWANZA: NYUMBANI

| | |
|---|---|
| SFX | SAUTI ZA USIKU |
| ANGELA | (Anazungumza peke yake) Mm kwa hiyo Pinto anataka mie niishi nae, haya nayo mazito, lakini inabidi nijue haya matokeo yanamaanisha nini kwangu na kwa huyo Pinto mwenyewe kwa sababu lazima itakuwa yeye kaniambukiza. Hakujakuwa na mtu mwingine katika maisha yangu. Yeye ndo wa kwanza, lo - nitafanyaje mie tazama mikono inavyonitetemeka.Yule daktari majoro kule kliniki ya matula hajanambia chochote, siwezi kumwambia mamangu, anajua kwamba nina mimba lakini moyo wangu wanambia nisimueleze cho chote kuhusu kupima HIV. Lo nafikiri nikimwambia itakuwa kasheshe, oohh mtoto |

| | |
|---|---|
| | anacheza tumboni, lo najiogopea mie sijui nifanyeje lazima nizungumze na mtu jamani, au ntashikwa na kichaa mie. |
| SFX | SAUTI ZA MAKARATASI |
| ANGELA | Hapa imeandikwa… (anasoma) yupo mtu anayeweza kukusaidia saa 24 kila siku kwa kukupa mafunzo, ushauri na kukueleza wapi pa kwenda ahaaa sasa afadhali hii, nikipiga simu hii ya kuomba usaidizi kwa wenye ukimwi, hawataniona, si nitakuwa nazungumza kwenye simu. Nafikiri itakuwa rahisi kuzungumza na mtu nsiyemfahamu na wala nisiyemuona. |
| SFX | SAUTI YA SAA |
| ANGELA | Lo - saa tatu, mama kalala saa hizi, naam huu sasa ndo wakati wa kufanya mambo Angela! yako wapi yale maswali? |
| SFX | SAUTI YA MAKARATASI |
| ANGELA | Ah! hizi hapa. |
| SFX | APIGA SIMU |
| ANGELA | Nambari ok, 0800012322… Lo jamani mbona mikono yatetema namna hii kasheshe... |

**SURA YA PILI: USIKU**

| | |
|---|---|
| SFX | Akiwa kitandani anahema |
| JET | (Yuko kitandani) Arrghh! Annie unaniumiza bwana Jees! |
| ANNIE | Nini tena Jet, kila mara unalalamika! |
| JET | Hebu washa kurunzi uniangalie nna nini Ouchhh |
| ANNIE | Kuna kitu chekundu kama kipele hivi… kinauma? |
| JET | Alama nyekundu? sasa sina maumivu lakini lo ilikuwa inauma kweli! |
| ANNIE | Kuna alama nyingine, ziko kadhaa. |
| JET | Na leo asubuhi nilipokuwa nakojoa nilihisi maumivu makali kweli kweli, umeniambukiza. |
| ANNIE | Eti nini? wasemaje? Kwa nini wasema hivyo? |
| JET | Nyinyi wanawake hamuwezekani! |
| ANNIE | Aha hiyo ndo tabia yenu wanaume: kila mara mnawalaumu wanawake kwa kila kitu, kwani mnafikri tunaambukizwa na kina nani? Kutoka kwa wanaume! |
| JET | Eeh! ninaona usaha wa ajabu. |
| ANNIE | Hmmm ikiwa ni kile ninachokifikiria mimi basi ni... |
| JET | Unamaanisha nini? |

ANNIE Kama ni maradhi za zinaa...
JET Nini, eti maradhi ya zinaa? Wasema nina maradhi ya zinaa?
ANNIE Hapana nasema ikiwa…
JET Na inakuaje unajua mengi kuhusu hali hii eh?
ANNIE Jamani Jet, si kuna mabango yamewekwa kila mahala kliniki, tena usisahau nakwenda mara kwa mara kliniki kwa ajili ya kuchukua tembe zangu za kujikinga kupata mimba na isitoshe mie najua kusoma, kuna maelezo kila mahala.
JET Ikiwa wewe umeniambukiza maradhi haya nitaaa…
ANNIE (kwa upole) Ikiwa nimeambukizwa basi nafikiri tunabidi twende pamoja kliniki au wasemaje?
JET Wewe... sendi kokote ...
ANNIE Na kwanini iwe hivyo? Kwa nini nyie wanaume mnaogopa madaktari?
JET Siogopi, nani kasema naogopa mpumbavu nini... mimi kawaida nakwenda kwa mganga wa kienyeji… hiyo ndo kawaida yangu na nitaendelea hivyo. Nyie wanawake nyote mnakwenda kliniki ya matula, mimi siwezi kwenda huko - sababu naweza kuonekana na mtu anayenifahamu.
ANNIE Kwa hivyo unaogopa usionekane na mwanamke mwingine? Kwa nini Jet? Una mwanamke mwingine sio?
JET Sasa Annie naona unakwenda mbali unaleta utoto.
ANNIE Ndio Jet, kwa sababu maradhi ya zinaa yanatokea huko, ukilala lala na wanawake kila aina basi matokeo yake ni haya
JET (Akitoa vitisho) Chunga mdomo unayoyazungumza, kabla hujashtumu mimi umesikia.
ANNIE Ouch Jet nyamaza usiendelee, umeshaniumiza...
JET Basi fikiria unachokisema kabla hujafugungua mdomo wako... (kimya kiasi) hata hivyo hakuna ubaya kwenda kwa mganga.
ANNIE Hapana Jet, magonjwa ya zinaa yahitaji matibabu ya hospitali.
JET Alaaa kwa hivyo unafahamu kila kila, au umeshawahi kupata maradhi haya sio!
ANNIE Aghh Jet bwana nimetubu, nitakwenda kliniki ya mjini ambako hakuna mtu anayenijua, wewe fanya unavyoona ni sawa.
JET Ooooooohhhhh hebu niingie chooni haraka oooohhh

inachoma kweli ooooohhhh

**SURA YA TATU: KWA MGANGA**

SFX MCHANA, MUZIKI WA KIASILI
MGANGA Hii itakusaidia kuondoa vipele hivyo jipake mara tatu kwa siku baada ya kuoga sawa
JET Asante. Je kuhusu maumivu nnapokojoa... kwa sababu bado nna maumivu mabaya sana.
MGANGA Wanaume wote wanaokuja hapa kutafuta matibabu wanatumia hiyo dawa inaitwa IMBIZA, wanasema inawafaa, wanasema inasafisha kila kitu na inawapa nguvu.
JET IMBIZA? niinywe yote?
MGANGA Hapana, hapana kijana… kijiko kimoja kila usiku inaponya kila kitu, hata ukimwi
JET (kwa mshtuko) Lakini mie sina ukimwi ni maradhi ya zinaa tu
MGANGA Usijali hiyo inaponya kila kitu... haya lete mia tatuuu
SFX Anahesabu pesa, MUZIKI WA KIENYEJI CHINI KWA CHINI

**SURA YA NNE: CHUMBANI**

ANGELA (Akiwa na furaha) Nakwambia Djamila huyo bwana akanisaidia kweli!
DJAMILA (Akicheka) Ai Angela jamani unafikiri kwa njia ya simu hiyo ya kutoa usaidizi unafikiri imeosha.
ANGELA Ndio, lakini alinieleza mambo vizuri nikaelewa, niliandika kwenye karatasi, alisema (anasoma) kujenga nyumba nzuri itakayokuhifadhi kutokana na jua, baridi, upepo na mvua unahitaji vifaa vizuri, msingi madhubuti na paa pamoja na kuta madhubuti vile vile. Jifikirie mwili wako kama ni nyumba. Ukipewa vifaa vinavyostahili unaweza pia ukajilinda kutokana na vidudu na virusi ambavyo hushambulia mwili. Alinambia nijiandae kufanya mabadiliko makubwa katika mtindo wa maisha yangu.
DJAMILA Kama nini Angela?

| | |
|---|---|
| ANGELA | Nile matunda kwa wingi na mboga mboga, maziwa, asali, njugu, mahindi, na nafaka pamoja na nyama. |
| DJAMILA | Heeee Angela, vitu vyote hivyo si itakuwa gharama kubwa, utaweza? |
| ANGELA | Nitajitahidi kuweka fedha kwa kujizuia kununua peremende na vyakula vya mahotelini, na pia niliambiwa mazoezi ni muhimu, na hasa baada ya kujifungua! |
| DJAMILA | Wow, kweli hayo ni mabadiliko makubwa katika maisha. |
| ANGELA | Nafikiri Djamila inahitaji tu niwe jasiri vya kutosha ili kufanya virusi hivi visinitawale kama nilivyoambiwa |
| DJAMILA | Lakini sio janga lako peke yako, huo ni ukweli unaopasa kuangaliwa na kila mtu, nitajiunga ntakuunga mkono, tutafanya sote mazoezi tutakula sote vyakula vya afya. |
| ANGELA | Bahati mbaya lakini Djamila mie nitahamia kwa Pinto jumapili |
| DJAMILA | Ah, nilikuwa nimeshasahau si haba lakini amekubali kubeba jukumu kwa yale yaliyotokea, lakini mtaishi pamoja bila ya kuoana? |
| ANGELA | Sijui wala sina habari nini kitakachotokea. (kimya) Lakini kitu kizuri ni kwamba huo mji nnakohamia ni karibu na kliniki ya mjini. Na pia kuna upande wa kuwahudumia wajawazito, nimetumwa huko na wale watu wa kutoa huduma kwa wenye ukimwi kwa njia ya simu. Kwa hivyo nitapata huduma nzuri ya ushauri nasaha kwa ajili yangu na mwanangu. |
| DJAMILA | Yaani siamini utakuwa mama hivi karibuni! |
| ANGELA | Na kwa maana hiyo mama mzuri ambaye atazungumza na mwanawe! We subiri tu utaona! |
| DJAMILA | Unaondoka saa ngapi? |
| ANGELA | Baada ya kanisa, usikasirike nitarudi. Nitakuwa na miaka 18 katika muda wa miezi kadhaa, halafu nitakuwa na uhuru wa kufanya nitakavyo. Pengine Pinto atakuwa mtu mzuri, tunaweza kujifunza kupendana... |
| DJAMILA | (Anacheka) Sasa umeanza kuzungumza kama mamangu, akinambia juu ya ndoa ya kunipangia. |
| ANGELA | Swadakta! |
| DJAMILA | (Abadilika na kuwa mkali) Natamani kama angeona jinsi kakake alivyo kama kupe. |
| ANGELA | Eh nani huyo? |
| DJAMILA | Nani mwingine, si mjomba Imrat... hata siwezi kuelezea |

nakwambia yuko hapa na hapa. na kila mtu katika familia anajifanya kama haoni. Wako kama mbuni na vichwa vyao wamevizika mchangani. (kimya) sasa mimi nitafanya nini?

**Hitimisho**

Malaika wa kila mtu ni mchezo uliotungwa na ROMIE Singh na kuhaririwa na Saumu Mwasimba.

Hadi hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi cha sikiliza ujifunze. Jiunge nasi mara nyingine ambapo utasikia jinsi Tom anavyokabiliwa na changamoto kutoka kwa marafiki zake wanaomtaka ajionyeshe jinsi alivyo mume lakini mwishowe anajikuta akimuelezea Annie kinachomkera.Pia tutaungana na Angela ambaye anakaribia kupiga hatua katika maisha yake mapya.

Kumbuka ikiwa unataka kusikiliza tena mchezo huu au kuna marafiki ambao wangependa kuusikia mchezo huu tembelea tovuti yetu www.dw.de mkwaju lbe.

KWA HERI.